JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII

MAMLAKA YA CHAKULA NA MADAWA TANZANIA

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

UFAFANUZI KUHUSU VYAKULA VYA WATOTO VILIVYOWAHI KUZUIWA NA AMBAVYO VIMEIDHINISHWA KUUZWA HAPA NCHINI

1. Lactogen 1 toleo Na. 73100179 L1

Mnamo Septemba 20, 2008 Mamlaka iliutangazia umma kuwa inaondoa sokoni bidhaa ya vyakula vya watoto aina ya Lactogen 1 yenye toleo Na. **73100179 L1** iliyotengenezwa na kufungashwa tarehe 6 Novemba, 2007 na kampuni ya Nestle ya Afika Kusini. Uamuzi huu ulifikiwa baada ya maziwa haya kugundulika kuwa na kiasi kikubwa cha madini ya chuma. Taarifa hii ilitokana na tangazo la kampuni ya Nestle ya Afrika Kusini kwamba maziwa haya yalikosewa katika uchanganyaji na hivyo kusababisha kiwango cha madini ya chuma katika maziwa hayo kuzindi kile kinachokubalika.

Mamlaka ilifanya ukaguzi katika maduka mbalimbali ya vyakula vya watoto hapa nchini na kuondoa bidhaa za toleo tajwa. Pia Mamlaka iliimarisha ukaguzi katika vituo vya mipakani kuhakikisha kuwa bidhaa hizi haziingii nchini na zilizokwisha ingia katika soko la Tanzania haziwafikii walaji.

Toleo Na. **73100179 L1** la bidhaa za Lactogen 1 iliyotengenezwa na kufungashwa tarehe 6 Novemba, 2007 na kampuni ya Nestle ya Afika Kusini ndio pekee iliyokuwa na matatizo. Matoleo mengine hayakuwa na tatizo na hivyo vibali vya uingizaji wa bidhaa hizi vinaendelea kutolewa.

2. Maziwa na bidhaa za maziwa toka nchini China

Septemba 23, 2008 Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), ilisitisha kutoa vibali vya uagizaji na usambazaji wa maziwa na bidhaa zenye viambata vya maziwa kutoka China. Uamuzi huu ulitokana na taarifa kutoka mtandao wa kimataifa wa Mamlaka za Udhibiti wa Usalama wa Chakula wa Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), zilizoeleza kuwepo kwa tatizo la athari za figo kwa watoto nchini China waliokula vyakula vya watoto vilivyosindikwa kwa kutumia maziwa yenye kemikali aina ya *melamine*.

Kufuatia kutangaza juu ya usitishwaji wa uingizaji na usambazaji wa maziwa na bidhaa zenye viambata vya maziwa kutoka China, Mamlaka ilikusanya bidhaa mbalimbali za maziwa na mazao yake kutoka katika soko kwa lengo la kufanya uchunguzi wa *melamine*. Kati ya bidhaa 94 zilizochukuliwa katika soko, bidhaa moja (Golden Bell Instant Milk Powder) yenye uzito wa tani 34 kutoka nchini China iligundulika kuwa na *melamine* kwa kiasi hatarishi kwa afya ya mlaji. Maziwa hayo yaliteketezwa kwa mujibu wa Sheria. Pia Mamlaka kupitia vyombo mbalimbali vya habari (Televisheni, magazeti na redio) ili washauri wananchi kuacha kununua maziwa na bidhaa zitokanazo na maziwa ambazo hazina lebo au zenye lebo zinazotiliwa mashaka.

Hivi karibuni, Mamlaka imeamua kuondoa amri ya kusitisha uingizaji nchini wa maziwa na bidhaa za maziwa kutoka China kwa angalizo kuwa:

a. Ukaguzi wa bidhaa hizo na uchunguzi wa maabara dhidi ya kemikali ya *melamine* kwa kila shehena ya bidhaa hizo utafanyika kwa kila shehena inayoingia nchini.
b. Shehena hizo zitazuiliwa kusambazwa hadi hapo majibu ya uchunguzi wa kimaabara yatakapotoka na Mamlaka kujiridhisha kwamba bidhaa hiyo haina *melamine*.
c. Udhibiti huu utafanyike kwa muda wa mwaka mmoja ili kujiridhisha kwamba udhibiti wa *melamine* huko China umeimarika na usalama wa mlaji unalindwa. Baada ya hapo uchanganuzi utafanyika kuhusiana na matokeo ya uchunguzi wa mwaka mzima na kuchukua hatua kulingana na tathmini hii.

Uamuzi huu unatokana taarifa tulizopokea kutoka Ofisi ya Uchumi na Biashara ya Mwakilishi wa Jamhuri ya watu wa China nchini Tanzania yaliyowasilishwa TFDA kimaandishi kuihakikishia kwamba tatizo la uchafuzi wa maziwa na kemikali ya *melamine* nchini China limekwisha

3. Lactogen 1 na Nido 1 kutoka Afrika Kusini

Tarehe 1 Desemba 2008, Mamlaka ilisitisha kwa muda usajili, uingizaji na matumizi ya maziwa ya Lactogen 1 na Nido 1 kutoka Afrika Kusini. Uamuzi huu ulitokana na taarifa kutoka jimbo la Kwazulu Natal Afrika ya Kusini zilizoeleza kuwepo kwa tatizo la uchafuzi wa maziwa ya Lactogen 1 toleo Na. 82050179L1 la tarehe 23 Julai 2008 na NIDO 1 toleo Na. 81790181S02E1M la tarehe 27 Juni 2008 nchini Afrika Kusini uliotokana na kemikali iitwayo *melamine*.

Kufuatia kusitisha kwa muda kwa usajili, uingizaji na matumizi ya maziwa aina ya Lactogen 1 na Nido 1 kutoka Afrika ya Kusini, Mamlaka ilifanya ukaguzi katika maduka mbalimbali ya vyakula vya watoto hapa nchini kuhakiki kama bidhaa za toleo tajwa zimeingia nchini ambapo ilibainika kuwa toleo tajwa halikuingia nchini. Aidha Mamlaka iliendelea kuimarisha ukaguzi katika vituo vya mipakani ili kuhakikisha kuwa bidhaa hizi haziingii nchini.

Vilevile Mamlaka imeamua kuendelea kuruhusu uingizaji nchini wa maziwa ya watoto ya Lactogen 1 yanayotengenezwa Afrika Kusini ambayo yamesajiliwa na

TFDA. Mamlaka haijapata maombi ya kuingiza nchini maziwa aina ya NIDO , hivyo bidhaa hii haitarajiwi kuwa nchini. Ni muhimu kutofautisha kati ya maziwa ya Watoto aina ya NIDO1 na maziwa ya unga ya kawaida ambayo yameidhinishwa na Mamlaka kwa matumizi ya watu wote.

4. Maziwa ya watoto wachanga aina ya S-26 1 yaliyotengenezwa na kampuni ya Pharmacare Ltd. ya Afrika Kusini

Tarehe 27 Agosti 2009 Mamlaka ya Chakula na Dawa ilizuia matumizi ya maziwa ya watoto wachanga aina ya S-26 1 yaliyotengenezwa na kampuni ya Pharmacare Ltd. ya Afrika Kusini. Hii ni baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wazazi wa watoto waliodhurika kwa kuumwa tumbo, kutapika na kupiga chafya baada ya kula maziwa hayo. Bidhaa tajwa zilifanyiwa uchunguzi na kugundulika kuwa na kiwango kikubwa cha tindikali huru za mafuta (*free fatty acids*) na chemikali aina ya *peroxide* hali iliyoashiria kuharibika kwa mafuta yaliyokuwemo katika maziwa hayo.

Mamlaka iliwatahadharisha wananchi wote kutokutumia maziwa hayo na kutoa taarifa watakapobaini kuwepo kwa maziwa hayo sokoni. Pia wafanyabiashara wote wa maziwa hayo waliagizwa kutoa taarifa za kiasi cha maziwa walichonacho katika Ofisi za TFDA Makao Makuu au Kanda na Ofisi za Afya za Mikoa na Halmashauri ili kuwezesha kuondolewa kwa maziwa hayo sokoni.

Katika ukaguzi uliofanyika nchi nzima, katika maduka na maghala ya vyakula, ikiwa ni pamoja na yale yaliyotuhumiwa kuwa na maziwa hayo. Katika ukaguzi huo jumla ya makopo 40,040 ya maziwa ya S 26 toleo Na 502317 na 505620, yenye madini ya chuma ya ujazo wa gramu 400 kwa kila kopo yaliyotengenezwa na Kampuni Pharmacare Ltd, Woodmead-Sandton yalikutwa sokoni na sampuli zake kuchukuliwa kwa uchunguzi zaidi.

Baadhi ya maziwa hayo yalishateketezwa na kwa yaliyobakia, taratibu za uteketezaji zinaendelea kufanyika.

Kwa kuzingatia kuwa maziwa ya watoto ya S-26 1 bado hayajasajiliwa na kuwa maziwa hayo hayana vibali usitishwaji wa uingizaji na usambazaji wa maziwa hayo utaendelea. Mamlaka inawataka waingizaji wa maziwa haya kwa kushirikiana na Msindikaji wafanye usajili wa maziwa ya S 26 1

5. **Orodha kamili ya maziwa ya watoto yaliyoidhinishwa na TFDA**

Jedwali hapa chini linaonesha aina zote za maziwa ya watoto ambazo zimeidhinishwa na TFDA kuuzwa hapa nchini

Jedwali : Orodha ya maziwa ya watoto wachanga yaliyoidhinishwa na Mamlaka

Sn	Jina la Maziwa	Nchi inakotoka	Kampuni iliyosajili
1	Lactogen 1 Infant Formula	Afrika Kusini	Nestle Sea Trading , Box 105665, Dar es Salaam
2	Lactogen 2 Follow up formula	Afrika Kusini	Nestle Sea Trading , Box 105665, Dar es Salaam
3	Lactogen 1 Infant Formula	Ufaransa	Nestle Sea Trading , Box 105665, Dar es Salaam
4	Lactogen 2 Follow up formula	Ufaransa	Nestle Sea Trading , Box 105665, Dar es Salaam
5	NAN1 Infant Formula	Afrika Kusini	Nestle Sea Trading , Box 105665, Dar es Salaam
6	NAN2 Follow up formula	Afrika Kusini	Nestle Sea Trading , Box 105665, Dar es Salaam
7	NAN1 Infant Formula	Uholanzi	Nestle Sea Trading , Box 105665, Dar es Salaam
8	NAN2 Infant Formula	Ufaransa	Nestle Sea Trading , Box 105665, Dar es Salaam
9	Cow bell Infant Formula	Ufaransa	Promasidor (T) PTY, P.O.Box 40580, Dar es Salaam

6. Matokeo ya ukaguzi uliofanywa na TFDA hivi karibuni kufuatilia vyakula visivyoidhinishwa

Hivi karibuni TFDA ilifanya ufuatiliaji sokoni kubaini vyakula ambavyo vimeingizwa nchini bila kibali.

TFDA ilibaini kuwepo sokoni kwa aina mbalimbali za vyakula ambavyo vimeingizwa na kusambazwa bila idhini ya Mamlaka. Kati ya vyakula hivyo ni Maziwa ya watoto aina za SMA, Nursoy, Isomil, Infacare, Ifasoy, Nutrien Optium, Cow & Gate na aina zote za maziwa ya S-26. Maziwa hayo yalizuiwa kuuzwa hadi utaratibu wa sheria utakapofuatwa.

Aidha TFDA imefanya kikao na waingizaji, wasambazaji na wauzaji wa maziwa ya watoto wachanga na kuwaelekeza juu ya miongozo, kanuni na sheria za udhibiti

wa usalama na ubora wa vyakula hivyo. Wasambazaji hao wamekubaliana na utaratibu wa kisheria wa kupata kibali kutoka TFDA.

Hivyo, watumiaji wote wa maziwa wanatakiwa kutumia maziwa yaliyoko katika orodha ya jedwali hapo juu. Ikiwa kama watumiaji watabaini maziwa mengine nje ya orodha hii, ni vizuri wajiridhishe kupitia TFDA au wawakilishi wa TFDA kama maziwa hayo yana kibali halali cha TFDA kabla ya kutumia. Ikumbukwe kwamba TFDA inaendelea kusajili maziwa mengine kadri ya maombi yanavyoletwa siku hadi siku.

Imetolewa na:

Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Chakula na Dawa(TFDA),
Barabara ya Mandela,
Mabibo-External,
S. L. P 77150,
Dar es Salaam.
Simu: 255 22 2450512/ 2450751/ 2452108
Nukushi: 255 22 2450793
Barua pepe: info@tfda.or.tz
Tovuti: www.tfda.or.tz

- TFDA – Kanda ya Ziwa,
  Mtaa wa Nkurumah,
  S.L.P. 543,
  Mwanza.
  Simu: +255 28 2500733
  Faksi: +255 28 2541484
  Barua Pepe: mwanza@tfda.or.tz

- TFDA – Kanda ya Kaskazini,
  Mtaa wa Sakina,
  S.L.P. 16609,
  Arusha.
  Simu: +255 27 2547097
  Faksi: +255 27 2547098
  Barua Pepe: arusha@tfda.or.tz

- TFDA – Nyanda za Juu Kusini,
  Jengo la Mkoa la Mifugo,
  S.L.P. 617,
  Mbeya.
  Simu: +255 25 2504425
  Simu: +255 757 644146
  Barua Pepe: mbeya@tfda.or.tz

- TFDA – Kanda ya Mashariki,
  Jengo la Makao Makuu ya Mamlaka ya TFDA,
  Barabara ya Mandela,
  Mabibo-External,
  S.L.P. 77150,
  Dar es Salaam.
  Simu: +255 22 2450512/2450751/ 2452108
  Nukushi: +255 22 2450793
  Barua Pepe: info@tfda